HOTUBA YA WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI
PROF. MARK J. MWANDOSYA (MB).
KWENYE MKUTANO MKUU WA 11 WA MWAKA WA MAMLAKA ZA MAJISAFI NA MAJITAKA MIJINI - 16/04/2009 MJINI BABATI

Mhe. Henry Shekifu, Mkuu wa Mkoa wa Manyara,

Bw. Wilson Mukama, Katibu Mkuu, Wizara ya Maji na Umwagiliaji,

Eng. Christopher Sayi, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji na Umwagiliaji

Bw. Samuel Lupimo, Kaimu Mkurugenzi wa Maji Kibiashara

Ndugu Simon Sayore, Mwenyekiti wa Bodi ya EWURA

Ndugu Haruna Masebu, Mkurugenzi Mkuu wa EWURA

Ndugu Simon Mbesere, Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Babati,

Ndugu Wenyeviti wa Bodi za Mamlaka za Majisafi na Majitaka Mijini,

Ndugu Wakurugenzi na Wataalam kutoka Wizara ya Maji na Umwagiliaji,

Ndugu Viongozi mbalimbali wa Mkoa wa Manyara,

Ndugu Watendaji Wakuu wa Mamlaka za Majisafi na Majitaka Mijini,

Ndugu Wageni waalikwa,

Ndugu Wana habari,

Mabibi na Mabwana.

1. Utangulizi

Natanguliza shukrani zetu kwa Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kufikia siku ya leo na kukutana hapa Mjini Babati. Kwa niaba ya Wizara yetu ya Maji na Umwagiliaji, na kwa niaba yangu Mwenyewe, nachukua fursa hii kuwashukuru wote mlioitikia wito wa kuja kushiriki katika mkutano huu muhimu. Nikiwa Waziri mwenye dhamana katika sekta hii ya maji nawakaribisha washiriki wote wa mkutano huu ili tuweze kujadili masuala muhimu ikiwa ni pamoja na mafanikio, changamoto zinazotukabili na mikakati inayotakiwa kufanyika. Lengo letu ni kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira kwa wananchi waishio mijini na vijijini.

Ndugu Wajumbe, hapo awali mlikubaliana kwamba mkutano huu ungefanyika Arusha. Mikutano mingi ya kitaifa na kimataifa hufanyika Arusha. Ni kweli, kwa maana ya mikutano Arusha imejengwa vizuri. Lakini Tanzania ni zaidi ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza au Morogoro. Ni vema tukaipa changamoto kama hii ya mikutano mikubwa, miji yetu mingine ili nayo ijipime katika kuwa wenyeji wa mikutano. Hivyo basi, nilitumia mamlaka ya Waziri ya kutoa maelekezo ya kijumla au mahsusi kuamua mkutano wetu uwe Babati.

Ndugu Wajumbe, Naomba nitumie nafasi hii kuushukuru uongozi wa mkoa wa Manyara ukiongozwa na Mkuu wa Mkoa Mheshimiwa Henry Shekifu kwa kutukaribisha kwenye mkoa wenu ili tuweze kufanya mkutano huu muhimu katika kuendeleza sekta ya maji nchini. Nikiwa Mwenyekiti wa Mkutano huu wa Kumi na Moja (11), narudia kusema naamini Babati itatuwezesha kutimiza lengo lililotuleta hapa.

2. Malengo ya Kitaifa

Ndugu Wajumbe, Malengo ya Kitaifa katika Sekta ya Maji yameainishwa vizuri kwenye Ilani ya Uchaguzi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2005. Yanazingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Malengo ya Maendeleo ya Milenia na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA). Utekelezaji wa Dira hiyo umegawanywa katika malengo ya muda mfupi (Ilani na MKUKUTA) na muda wa kati. Katika muda wa kati, Serikali imedhamiria kutekeleza Malengo ya Kimataifa ya Milenia, hususan lengo namba 7 ambalo kwa sekta ya maji ni kupunguza kwa asilimia 50 idadi ya watu wasio na huduma ya majisafi na salama na huduma ya usafi wa mazingira, na kuweka mfumo shirikishi wa usimamizi wa rasilimali za maji ifikapo mwaka 2015. Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2005 ibara ya 67 (a) imetoa malengo ya majukumu yaliyo mbele yetu katika kipindi cha muda mfupi. Malengo hayo ni yafuatayo;

"Kuwawezesha wananchi mijini na vijijini kupata maji safi, salama na ya kutosha kwa matumizi yao..... na kuwafikishia huduma hiyo asilimia 90 ya wakazi wa mijini na asilimia 65 ya wakazi vijijini ifikapo mwaka 2010",

Ibara hii inatilia umuhimu wa kuwapatia wananchi majisafi, salama na ya kutosha kwa matumizi ya kila siku karibu na makazi yao. Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika hotuba yake ya kufungua Bunge la Tanzania tarehe 30 Desemba, mwaka 2005, ameweka bayana kilio cha wananchi kuhusu maji;

"Tatizo la maji ndicho kilio kikubwa cha Watanzania mijini na vijijini. Ndiyo kero nambari wani. ..... Serikali ya Awamu ya Nne inakusudia kulikabili tatizo hili ..... Itaweka msukumo mpya katika kuwawezesha wananchi wengi zaidi mijini na vijijini kupata maji salama" Maneno niliyoyanukuu ni mazito, na changamoto muhimu kwetu.

Ndugu Wajumbe, Katika kutekeleza malengo na majukumu yetu tunaongozwa na Sera ya Maji ya mwaka 2002. Pamoja na mambo mengine, sera ina madhumuni ya kuwezesha uendelezaji na usimamizi endelevu wa utoaji huduma ya majisafi na uondoaji majitaka kwa wakazi wa mijini. Madhumuni hayo yatafikiwa kwa kuweka malengo na kutoa miongozo na vigezo na viashiria vya utekelezaji wa shughuli zinazofanywa na Mamlaka hizi na watekelezaji wengine. Azma ya Serikali katika kuboresha huduma ya Majisafi na Uondoaji wa Majitaka Mijini, imo katika Sera ya Maji ya Mwaka 2002. Sera inalenga katika masuala yafuatayo:

(i) Kutoa mwongozo wa namna ya kuendeleza na kusimamia huduma ya majisafi na majitaka mijini kwa ufanisi.

(ii) Kuweka mazingira mazuri yatakayoivutia sekta binafsi pale inapowezekana kuwekeza katika kutoka huduma ya majisafi na uondoaji majitaka mijini.

(iii) Kuhakikisha kuwa upo muundo mzuri wa kitaasisi unaovipa vyombo vya uendeshaji huduma ya majisafi na majitaka mijini madaraka ya kujiendesha kibiashara.

(iv) Kuwa na mfumo madhubuti na wenye ufanisi katika ukusanyaji maduhuli yatokanayo na mauzo ya majisafi na uondoaji wa majitaka na hivyo kuongeza mapato na;

(v) Kupunguza upotevu wa maji na kuboresha uondoaji wa majitaka.

Moja ya vyanzo muhimu katika utekelezaji wa sera ni sheria na taratibu zinazotokana na sheria. Hivi sasa mapitio ya sheria za maji, sheria ya Matumizi ya Maji ya mwaka 1974 (*Water utilization (Control and Regulation) Act,1974)* kuwa sheria ya *Usimamizi wa Rasilimali za Maji* na sheria ya Maji kifungu 272 (*Water works Act, Cap 272)* kuwa sheria ya *Majisafi na Usafi wa Mazingira,* yaliyokuwa yanaendelea yamefikia hatua za mwisho. Tunatarajia kuwasilisha miswada kwa mara ya kwanza bungeni katika kikao chake cha mwezi huu wa Aprili mwaka 2009. Miswada hii ni kuhusu mabadiliko makubwa kwenye sheria mpya ya maji na usafi wa mazingira yanahusu kuyaweka bayana majukumu ya Serikali za Mitaa na wananchi kutokana na usimamizi wa utekelezaji wa utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira, kuratibu mipango na usimamizi wa rasilimali kwenye Mamlaka za Maji (WSSAs) na Jumuia za Watumiaji (COWSOs). Kwa upande wa Tawala za Mkoa, Sekretariati za Mikoa zitahusika na masuala ya kutoa miongozo kwenye Serikali za Mitaa kuhusu huduma za maji na usafi wa mazingira, kufuatilia miradi na kutoa utalaamu wa kiufundi. Mabadiliko ya Sheria hii yatamruhusu Waziri mwenye dhamana kutangaza kuhusisha eneo zaidi ya moja nje ya mipaka ya kiutawala (*One or more Local Government Authorities*) kuunganishwa na kufanya kazi chini ya Mamlaka (Clusturing). Mabadiliko mengine ni pamoja na:

- Kutambua Jumuiya za Wananchi (*Community Owned Water Supply Organization - COWSO*) ili kumiliki na kuendesha miradi ya maji;

- Kuainisha majukumu ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ili iweze kutekeleza majukumu yake ya udhibiti ipasavyo;

- Kuunda Mfuko wa Taifa wa Maji *(National Water Investment Fund*);

- Kuanzisha bodi itakayohusika na utoaji wa leseni kwa wahandisi, mafundi na mafundi mchundo watahusika katika ujenzi, usimamizi na uendeshaji wa miradi ya maji.

3. Mamlaka za Maji Mijini

Kama mnavyofahamu Mamlaka hizi zilianzishwa mwezi Januari, mwaka 1998 chini ya Sheria Na. 8 ya mwaka 1997. Kuna jumla ya Mamlaka 19 katika Makao Makuu ya Mikoa yote ya Tanzania Bara, ukiondoa DAWASA iliyoundwa na sheria na. 7 ya mwaka 1997 ambayo inahudumia Mkoa wa Dar es Salaam, maeneo ya Kibaha na Bagomoyo katika Mkoa wa Pwani. Katika ngazi ya wilaya kuna jumla ya mamlaka 109 ikijumuisha mamlaka 9 katika miji midogo

na 7 Miradi ya Kitaifa, Mamlaka hizi zote zipo katika daraja 'C'. Katika ngazi ya Mikoa, hadi sasa kuna jumla ya mamlaka 11 za daraja 'A' (Arusha, Dodoma, Iringa, Mbeya, Morogoro, Moshi, Mtwara, Mwanza, Shinyanga, Tabora, Tanga. Mamlaka 4 za daraja 'B' (Bukoba, Kigoma, Singida na Sumbawanga) na Mamlaka 2 za daraja 'C' (Babati na Lindi). Mamlaka hizi zipo katika makao makuu ya Mikoa.

3.1. Mashirika ya DAWASA na DAWASCO

Ndugu Wajumbe, Ninapenda kueleza uwepo wa mashirika ya DAWASA na DAWASCO. Shirika la DAWASA liliundwa rasmi tarehe 4 Aprili, 1997 kwa Sheria Namba **7** ya mwaka 1981 na marekebisho yake ya 1997 na 2001. Kwa mujibu wa marekebisho ya sheria hiyo ya DAWASA ilipewa majukumu mapya ya kuwa mmiliki wa miundombinu. Sheria hiyo imeipa mamlaka DAWASA kutoa huduma ya majisafi na kuondoa majitaka katika jiji la Dar es Salaam na miji ya Kibaha, Bagamoyo na maeneo yaliyo kandokando ya mabomba makuu ya majisafi kutoka katika mitambo ya Ruvu Juu na Ruvu Chini. Eneo hili lina jumla ya wakazi wasiopungua milioni 4.

DAWASCO ni Shirika la Uendeshaji wa Huduma ya Majisafi na Majitaka jijini Dar es Salaam lililoundwa kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika ya Umma ya mwaka 1992 kwa Notisi ya Serikali Namba 139 ya tarehe 20 Mei, 2005. Kuundwa kwa DAWASCO kulitokana na kusitishwa kwa mkataba kati ya Kampuni ya ***City Water Services Ltd*** na DAWASA. Mkataba huo ulihusu ***City Water Service Ltd*** kukodishiwa miundombuni ya majisafi na majitaka ili kuendesha shughuli za kusambaza majisafi na uondoshaji wa majitaka kwa wateja maeneo ambayo yako chini ya DAWASA.

Napenda kusisitiza kuwa muundo uliopo ulibuniwa kwa makusudi ya kuyapa mashirika haya mawili majukumu yasiyofanana lakini yanayotegemeana. Kutokana na mazingira halisi ya Jiji la Dar es Salaam na ukubwa wake na changamoto zilizopo kwa sasa, sheria iliyounda mashirika haya mawili itaendelea kubaki kama ilivyo kwa sasa.

Kwa kutumia uwezo wa Mamlaka kubwa, katika hatua za kuongeza ufanisi, katika utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira katika miji midogo kama ilivyoainishwa katika Mkakati wa Maendeleo wa Sekta ya Maji, (*National Water Development Strategy*), Wizara kwa sasa hivi kupitia Mshauri mwelekezi wanafanya utafiti wa namna bora ya usimamizi wa pamoja wa uendeshaji wa Mamlaka ndogo (*Clustering*). Kazi hii inatarajiwa kukamilika mwezi Agosti mwaka huu 2009 na kwa kuanzia tutaanza na Mamlaka mbili kwa majaribio (*pilot*) ambapo mafanikio yake yatawezesha Mamlaka zingine kuunganishwa.

3. Usimamizi wa Mamlaka za Maji Mijini

Ndugu Wajumbe, Wizara imeendelea kusimamia kwa karibu utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Majitaka zote za Miji mikuu ya Mikoa, Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo ndani ya Wilaya

na Miradi ya Kitaifa (*National Projects*). Mamlaka za miji hii hutuma Wizarani taarifa za utekelezaji kazi kulingana na Mkataba wa Makubaliano kila mwezi, robo mwaka, na mwaka. Utumaji wa taarifa hizi umeboresha mahusiano kati ya mamlaka na Wizara jambo ambalo kwa kiasi kikubwa limerahisisha kazi ya usimamizi. Katika usimamizi huu, pamoja na taarifa ya utendaji, Wizara imekuwa ikifanya Tathmini ya Bodi za Maji za Mamlaka ambazo ndio zenye jukumu la kusimamia Menejimenti zinazoendesha Mamlaka. Katika tathmini ya utendaji katika kipindi cha 2007/2008, taarifa nilizonazo kupitia tathmini iliyofanyika ni kuwa Bodi zote zimejitahidi kutekeleza majukumu yake kwa asilimia 70. Majukumu muhimu ya Mamlaka hizi pamoja na DAWASA ni kusambaza majisafi na salama na kuondoa majitaka kwa wakazi waishio mijini. Utekelezaji wa jukumu hili kubwa utawezesha kufikiwa viwango vinavyotakiwa endapo Mamlaka hizi zitakuwa na mapato ya kutosha kuweza kugharamia shughuli zote za uendeshaji wake na kuwa na bakaa ambayo itatumika katika kuwekeza kwenye miundombinu, kulinda vyanzo vya maji na kuboresha rasilimali zote za Mamlaka.

Kwa kushirikiana na Mamlaka, Wizara imeweza kuweka utaratibu mzuri wa utendaji katika Mamlaka hivyo kuchangia uboreshaji wa hali ya watumishi na tija kuongezeka kutokana na Mamlaka za daraja 'A' na 'B' kupanga na kuwalipa watumishi mishahara kutokana na makusanyo yao. Kuhusu watumishi wa Mamlaka za Daraja 'B' na 'C' hali zao pia zimeboreshwa kutokana na Bodi husika kupanga motisha mbalimbali kwa watumishi wao kutegemeana na makusanyo na kwa kuzingatia miongozo iliyopo. Hali hii kwa ujumla imesaidia kuboresha huduma ya maji katika miji yetu. Nazipongeza bodi zote kwa usimamizi mzuri na wenye tija.

5. Utendaji wa Mamlaka katika Mwaka wa fedha 2007/2008

Ndugu Wajumbe, Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2007/20078 Mamlaka zimeendelea kuboresha huduma ya Maji kwa kuongeza uzalishaji kutoka mita za ujazo **274,520** mwaka 2006/2007 hadi kufikia mita za ujazo **287,997.** Idadi ya wakazi wanaopata huduma ya Maji maeneo ya mijini kwa mwaka 2007/2008 imeendelea kuwa ni asilimia **80** sawa na mwaka 2006/2007. Ukusanyaji wa mapato ya Mamlaka umeongezeka kutoka Shilingi bilioni **24.76** mwaka 2006/2007 hadi kufikia Shilingi bilioni **29.87** mwaka 2007/2008. Mamlaka zimeendelea kudhibiti upotevu a maji ambapo kwa mwaka 2007/2008 upotevu umepungua na kufikia asilimia **37** ikilinganishwa na mwaka jana ambapo upotevu ulikuwa ni asilimia **39.7**

Kwa upande wa ukusanyaji madeni, mamlaka hazikufanya vizuri kwani deni limeongezeka kutoka shilingi bilioni **5.44** mwaka 2006/2007 hadi kufikia kiasi cha Shilingi bilioni **7.47** kwa mwaka 2007/2008. Kwa upande wa DAWASCO deni limepungua toka shilingi 25.5 bilioni. Changamoto kubwa kwa Mamlaka ni kuongeza ufanisi katika kukusanya maduhuli ili kuongeza mapato. Ufuatiliaji wa madeni kwa wateja binafsi na asasi za umma.

Kutokana na mradi unaoendelea wa kuboresha miundo mbinu jijini Dar es Salaam. Hali ya ubora wa maji na uzalishaji umeongezeka kutoka mita za ujazo **302,111** kwa siku mwaka 2006/2007 hadi kufikia mita za ujazo **306,307** kwa siku mwaka 2007/2008. Makusanyo ya maduhuli chini ya DAWASCO yameongezeka kutoka shilingi bilioni **17.5** mwaka 2006/2007 hadi kufikia shilingi bilioni **21** mwaka 2007/2008, ongezeko hili ni sawa na asilimia **20**.

Ndugu Wajumbe, Mamlaka zote zimefanyiwa ukaguzi wa hesabu (*Audited Accounts*) chini ya usimamizi wa Mkaguzi Mkuu wa Serikali (*Controller and Auditor General* (CAG)) kwa wakati na kupata cheti cha usahihi (*Certificate of Correctness – CoC*). Mwaka 2007/2008 Mamlaka zote katika ngazi ya mkoa zilipata vyeti safi (*Unqualified*), isipokuwa Mamlaka za DAWASA, DAWASCO, Dodoma na Singida. Hili ni jambo la kujivunia katika mamlaka zetu. Nawapongeza Watendaji pamoja na Bodi za Mamlaka ambazo zimepata vyeti safi. Huu ndio uongozi bora kwani mmeweza kusimamia vizuri Mapato na Matumizi ya fedha za Mamlaka zenu kwa manufaa ya wananchi. Kwa wale wenye hati zenye mashaka, nawaelekeza Wenyeviti wa Bodi husika kufuatilia kwa karibu watendaji wao ili hali hii isijirudie mwakani.

6. Utekelezaji wa Malengo katika Mkataba wa Makubaliano

Ndugu Wajumbe, Mkataba wa Makubaliano kati ya Wizara na kila Mamlaka (MoU) (2005 – 2008) ni mkataba wenye malengo na viashiria vinavyolenga kuongeza ufanisi katika Mamlaka. Msingi wa mkataba huu ulilenga katika kuhakikisha kwamba huduma ya Majisafi na Uondoaji wa Majitaka katika miji yetu inakuwa bora mwaka hadi mwaka ili tuweze kuyafikia malengo yaliyowekwa katika MKUKUTA (2010), Malengo Maendeleo ya ya Milenia (2015) na Malengo ya Kitaifa (2025).
Utekelezaji wa Mkataba huu umerahisisha usimamizi wa Mamlaka unayofanywa na Wizara kwani unaeleza wazi uelekeo wa Mamlaka katika utendaji wake. Ndani ya kipindi hiki cha miaka 3 tumeshuhudia huduma ya Majisafi na Majitaka ikiongezeka kwa kiwango cha kuridhisha. Katika kipindi hiki ufanisi katika mamlaka umepanda katika viashiria karibu vyote. Kazi kubwa iliyopo mbele yetu ya kuhakikisha ufanisi huu na malengo ya kitaifa ya kuboresha huduma ya maji yanafikiwa. Kwa muhtasari baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hiki cha miaka 3 ya utekelezaji wa Mkataba, ni kama ifuatavyo:

(i) Katika miji mikuu ya mikoa, idadi ya wakazi wanaopata huduma imeongezeka hadi kufikia asilimia **80** mwaka 2007/2008 ikilinganishwa na asilimia **78** katika mwaka 2005/2006 ambapo upatikanaji wa Maji umeendelea kuwa wastani wa masaa **18** kwa siku katika mfululizo wa vipindi vya miaka mitatu.

(ii) Mamlaka zimeweza kuongeza uzalishaji wa maji kutoka mita za ujazo **273,698** katika mwaka 2005/2006 hadi kufikia mita za ujazo **288,109** kwa siku katika mwaka 2007/2008.

(iii) Kwa upande wa majitaka, kumekuwa na ongezeko la wakazi waliounganishwa kwenye mfumo wa majitaka kutoka wastani wa asilimia **14** mwaka 2005/2006 na kufikia wastani wa asilimia **17** mwaka 2007/2008, sawa na asilimia 21.

(iv) Makusanyo ya maduhuli pia yameongezeka kutoka shilingi bilioni **21.4** mwaka 2005/2006 hadi kufikia shilingi bilioni **29.87** katika mwaka 2007/2008. Ongezeko hili limeziwezesha Mamlaka nyingi kutoa huduma nzuri pamoja na kuboresha na kuongeza mitandao ya majisafi kwenye maeneo yaliyokuwa hayana huduma.

Idadi ya wateja waliounganishwa kwenye mtandao wa maji imeongezeka kutoka **183,892** mwaka 2005/2006 hadi kufikia wateja **210,970** mwaka 2007/2008, sawa na asilimia **84** ya wateja wote

kwenye miji ya makao makuu ya mikoa waliofungiwa dira za maji. Ongezeko hili limewezesha kupunguza upotevu wa maji (*Unaccounted For Water) -(UFW)* kutoka asilimia **41** mwaka 2005/2006 hadi asilimia **37** mwaka 2007/2008.

Ndugu Wajumbe, kwa ujumla Mamlaka zimeendelea kufanya vizuri katika kufikia malengo yaliyowekwa kwenye mkataba wa makubaliano ya utendaji kati yao na Wizara ambapo mamlaka 6 za Mbeya, Arusha, Dodoma, Tanga, Moshi na Morogoro zimeweza kufikia malengo yaliyowekwa kwa asilimia kati ya 80 mpaka 100. Naupongeza uongozi wa Mamlaka hizi pamoja na Bodi zake kwa kazi nzuri waliyoifanya. Mamlaka nyingine zote zimefikia kati ya asilimia 50 hadi 80.

Ndugu Wajumbe, Mkataba (*Lease Contract*) wa Ukodishaji kati ya DAWASA na DAWASCO unaohusisha faini ya fedha kwa malengo ambayo hayakufikiwa, DAWASCO waliweza kufanya vizuri kwa kuvuka malengo katika viashiria vya Ukarabati wa mabomba na Ubora wa Majisafi yanayosambazwa kwa wateja. Kwa upande wa ufungaji wa dira za maji na ufanisi katika kukusanya maduhuri waliweza kufikia malengo kwa asilimia 52 na kwa upande wa kuunganisha wateja wapya wa majisafi hali haikuwa nzuri kwani waliweza kufikia malengo kwa asilimia 36 tu. Katika mkataba wa ukodishaji usiohusisha faini ya fedha kwa malengo ambayo hayakufikiwa, DAWASCO iliweza kufikia malengo kwa asilimia 18 tu, ijapokuwa ilivuka malengo katika viashiria vya kuongeza akaunti za Majisafi na Majitaka na kupokea simu za wateja. Malengo mengi ambayo hayakufikiwa ni yale ambayo yanaendana na kukamilika kwa mradi. Ni matarajio yangu, baada ya mradi kukamilika ifikapo mwezi Desemba 2009, hakutakuwa tena na sababu za msingi za kutokufikia malengo yaliyowekwa.

Ndugu Wajumbe, Malengo yaliwekwa kwenye Mkataba yakifikiwa, ndio yanaonesha mwelekeo wa kila mamlaka katika kukua ama kupandishwa daraja. Kutokana na utekelezaji wa malengo hayo na baada ya kutimia vigezo na viashiria tulivyokubaliana, na kwa kutumia mamlaka niliyonayo, nafurahi kuwataarifu kwamba kupitia Gazeti la Serikali *Government Notice* Namba **40** la tarehe **5 Desemba, 2008** Mammlaka za Musoma na Songea zimepandishwa daraja. Napenda nichukue nafasi hii kuzipongeza Bodi na Menejimenti za Mamlaka za Musoma na Songea kwa kupanda daraja kutoka 'B' kuingia daraja 'A' kuanzia tarehe **1 Julai, 2008**. Kulingana na taratibu zilizopo daraja 'A' maana yake ni kuelekea kujitegemea zaidi kwa kulipa gharama zote za uendeshaji na matengenezo pamoja na sehemu ya uwekezaji. Napenda kutoa changamoto kwa Mamlaka za daraja 'C' za Babati, Lindi na zilizopo ngazi za Wilaya na Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa kujitahidi katika kutekeleza malengo na kuhakikisha kwamba katika kipindi kifupi kijacho nazo zinapanda kutoka hapo zilipo mpaka kufikia Daraja "B" au "A", kwani wahenga walisema "Penye nia pana njia". Kuwepo kwetu hapa Babati ni Chachu ya babati kupanda daraja. Mafanikio ya Mkutano wetu wa 11 ni pamoja na kuisaidia Babati ipande daraja.

7. Mamlaka ya Udhibiti Huduma za Maji na Nishati (EWURA)

Ndugu Wajumbe, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (EWURA) kwa kushirikiana na Wizara Mamlaka imeweza kupitia na kuboresha zaidi Mkataba wa Makubaliano kati ya Wizara na kila Mamlaka kwa kipindi cha 2008 - 2011. Katika kuboresha Mkataba huu, baadhi ya viashiria vya utekelezaji vilivyoonekana kupitwa na wakati viliondolewa na vingine kuongezwa kutokana na umuhimu wake. Kwa kuzingatia majukumu ya EWURA, kama yalivyoainishwa katika Sheria ya EWURA, moja za kazi ya EWURA ni kutathmini utendaji katika Mamlaka wanazozidhibiti. Hii ni kuhakikisha kwamba huduma inayotolewa inalingana na thamani ya fedha inayotozwa *(value for money*). Hivyo basi, mbali na Malengo ya Utekelezaji *(Performance Contract)* yaliyokuwepo katika Mkataba wa awali, mkataba wa sasa umeboreshwa kwa kuyatambua majukumu ya EWURA kwa kuweka viwango mbalimbali vya ubora wa huduma. Malengo haya yatatathiminiwa na EWURA kila robo ya mwaka kwa kutumia makubaliano yaliyofikiwa kati ya EWURA na kila Mamlaka *(Perfomance Agreement*). Tathmini itawasilishwa katika Mkutano huu kila mwaka kabla ya kutangazwa.

Katika mwaka 2007/2008 EWURA ilitoa leseni za muda kwa Mamlaka **19** za makao makuu ya mikoa na kupitia maombi **23** ya kurekebisha bei za maji. Maombi **21** yalipitishwa. Mamlaka **31** za miji mikuu ya Wilaya na miji midogo ziliomba leseni ya muda. Hakuna hata moja iliyoweza kufikia vigezo vya kupata leseni hiyo. Hii ni changamto kubwa kwa Mamlaka hizi. Inabidi ziongeze jitihada ili zikidhi vigezo vya kujiendesha kibiashara na hivyo uwekezaji na kujenga uwezo unaohitajika.

8. Utendaji wa Mamlaka za Maji za Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa *(National Projects*)

Katika kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP) Mamlaka zilizopo ngazi ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa zilihamishiwa chini ya usimamizi wa Idara ya Majisafi Kibiashara (*Commercial Water Supply and Sewerage*). Nimeambiwa kwa mara ya kwanza tangu kuanzishwa mamlaka hizi, Idara imeweza kufanya tathmini ya awali ya kuangalia hali halisi ya huduma katika mamlaka hizi. Katika tathmini hii ya awali kati ya ya miji **109** ya makao makuu ya Wilaya, miji midogo na miradi ya kitaifa imeonyesha kwamba ni miji **72** tu ya makao makuu ya Wilaya, miji midogo **7** na miradi ya kitaifa **5** ndiyo yenye Bodi za maji zilizo hai. Kati ya miji yote ya makao makuu ya Wilaya, miji midogo na miradi ya kitaifa ni miji **40** tu ambayo ina mikataba ya makubaliano (MoU) kati ya Bodi na Wizara. Bado tunao wajibu wa kuhakikisha kwamba miji yote inakuwa na MoU kwa ajili ya usimamizi endelevu.

Hali ya huduma ya maji katika miji hii bado sio nzuri na inapishana sana. Kwa mfano Kahama (kabla ya mradi wa Kahama-Shinyanga) ni asilimia **2** tu ya wakazi waliokuwa wakipata huduma ya maji, wakati kwa mji wa Same ni asilimia **85**. Aidha upotevu wa maji kwa mji wa Kasulu ni aslimia **95** wakati mji wa Nzega ni asilimia **15**. Changamoto zinazoikabili miji hii ni pamoja na miundombinu chakavu, ukosefu wa watumishi wenye utaalamu pamoja na kutokuwa na utaratibu wa kutunza kumbukumbu na takwimu.

Pamoja na changamoto hizo katika kipindi cha mwaka 2007/2008, kiasi cha maji kilichozalishwa ni wastani wa mita za ujazo milioni **39.6** na makusanyo ya maduhuli yalifikia jumla ya shilingi bilioni **3.71** wakati matumizi yalikuwa shilingi bilioni **5.48**.

Ndugu Wajumbe, Kuna mamlaka **15** za miji midogo zimefanya vizuri ambazo ni; Tukuyu, Kyela, Itumba, Ngara, Liwale, Kibaya, Kondoa, Nzega, Kibondo, Njombe, Pangani, Mbinga, Namtumbo na Kasumulu. Katika hali ya kifedha inaonyesha mapato ni makubwa kuliko matumizi. Maji yanayopotea ni chini ya asilimia **50**, idadi ya watu wanaopata huduma ni zaidi ya asilimia **50** ya wakazi. Wizara itazisimamia kwa karibu na kuzijengea uwezo mamlaka hizi ili ziweze kupanda daraja kutoka C kwenda B au hata A na kuanza kutathminiwa kwa karibu zaidi kwa mtindo wa kibiashara.

9. Utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP)

Ndugu Wajumbe, Katika kuhakikisha kuwa tunafikia Malengo ya Milenia, Serikali iliandaa Mkakati wa kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA) ambao utekelezaji wake ni wa miaka mitano, mwaka 2005 hadi 2010. katika mkakati huo, Sekta ya maji imepewa jukumu la kuwapatia wananchi majisafi na salama, karibu na makazi yao, kwa kuongeza idadi ya wananchi wanaopata huduma hiyo vijijini kutoka asilimia **53.5** mwaka 2004/2005 hadi asilimia **65** na kwa maji mijini kutoka asilimia **74** mwaka 2004/2005 hadi asilimia **90** ifikapo mwaka 2010.

Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji iliendelea kutekeleza malengo mbalimbali katika eneo la kujenga uwezo *(capacity building)* wa uendeshaji na usimamizi wa kutoa huduma wa mamlaka zote ikiwa ni pamoja na zile ndogo. Eneo la uboreshaji wa miundombinu lilihusisha ukarabati na ujenzi *(capital investment)* wa miundombini ya Majisafi na Majitaka mijini. Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa programu hii ni kama ifutavyo;

(a) Kujenga Uwezo

- Ununuzi wa magari 10, pikipiki 40, Kompyuta 40 na Vifaa vya ofisi kwa ajili Mamlaka mbalimbali za Miji Mikuu ya mikoa ambayo ni Bukoba, Kigoma, Songea, Babati, Lindi, Mtwara, Musoma, Singida, Shinyanga na Sumbawanga.
- Kuwapata Wataalamu elekezi kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu, uchunguzi wa kina na usanifu wa miundombinu ya majisafi na majitaka katika mikoa ya Moshi, Babati, Shinyanga, Morogoro, Tanga, Lindi, Mtwara, Tabora, Sumbawanga na Dodoma.

(b) Ukarabati na Ujenzi wa Miundombinu ya Majisafi na Majitaka

- Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya Majisafi na Majitaka katika miji ya Mbeya, Iringa, Mwanza, Songea, Singida na Dar es salaam

Ndugu Wajumbe, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka husika waliendelea kusimamia ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya majisafi na majitaka katika miji ya Mbeya na Iringa. Utekelezaji wa mradi wa majisafi mjini Mwanza uliogharimu shilingi **bilioni 38** ulikamilika pamoja na mradi wa majisafi na majitaka mjini Songea uliogharimu **shilingi bilioni 36.** Usanifu kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya majisafi na majitaka uko katika hatua mbalimbali kwenye miji ya mikoa na wilaya.

Mradi mkubwa wa kutoa maji Ziwa Victoria na kupeleka miji ya Kahama na Shinyanga na vijiji 54 upo kwenye hatua za mwisho. Mradi huu umeigharimu serikali hadi sasa jumla ya shilingi bilioni 225. Fedha hizi zimetolewa na serikali kutoka kwenye bajeti.

Katika mwaka 2007/2008 jumla ya shilingi bilioni **123.22** zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali katika programu ndogo ya majisafi na majitaka chini ya Programu ya WSDP. Katika fedha hiyo kiasi cha shilingi bilioni **52,85** ikiwa ni mchango wa serikali na shilingi bilioni **70,37** ikiwa ni mchango kutoka kwa wahisani mbalimbali. Hadi kufikia Juni 2008, kiasi cha shilingi bilioni **97,81** zilitolewa na kutumika. Kwa mwaka wa fedha 2007/2008, Programu ndogo ya majisafi na majitaka ilipokea kiasi cha Shilingi bilioni **72.79** ambapo kati ya hizo, Shilingi Bilioni **5.57** zilitolewa kwa mamlaka ndogo 35 kwa ajili ya kusaidia kazi za kutoa matokeo ya haraka *(immediate works*). Shilingi bilioni **2.03** zilitolewa kwa ajili ya kulipia gharama za umeme na kusaidia kazi zenye matokeo ya haraka (immediate works) kwenye Miradi ya Kitaifa,shilingi bilioni 4.95 kusaidia utekelezaji wa kazi za Mamlaka daraja B na C na Shilingi Bilioni **58.73** zilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya miradi miwili ya Maji ya Kahama-Shinyanga, Songea, Mwanhunzi na Bariadi.

10. Maji na Mazingira

Ndugu Wajumbe, Sera ya Maji inasisitiza kuhusu Mamlaka za Majisafi na Majitaka mijini kuweza kumiliki maeneo kuzunguka vyanzo vya Maji ili kuweza kuvitunza, kuvilinda na kuhakikisha vyanzo hivyo vinaepukana na uharibifu wa Mazingira. Kasi ya kumiliki maeneo haya ni ndogo na haiendani na Malengo ya kuboresha upatikanaji wa maji kwa jamii kwani bila kuvilinda na kuvitunza vyanzo vya maji vilivyopo kuna hatari ya kuharibiwa, kukauka na kupotea kabisa.

Ongezeko la uzalishaji wa majisafi uliopo sasa hauendani kabisa na ongezeko la huduma ya uondoaji majitaka katika miji yetu. Takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa tangu mamlaka kuanzishwa mwaka 1998 hadi mwaka 2008 ni asilimia 17 tu ya wakazi waliounganishwa kwenye mfumo wa majitaka. Maeneo mengi katika miji yetu hayana mifumo mizuri ya uondoaji majitaka, kwani hata ile iliyopo ni midogo na haijaweza kuwafikia wakazi wengi. Idadi ya wateja waliounganishwa kwenye mtandao wa majitaka bado ni ndogo na husababisha Majitaka yanayozalishwa kutokana na matumizi ya Majisafi kubaki katika maeneo tunayoishi. Hali hii yaweza kuhatarisha hali ya usalama wa afya zetu kutokana magonjwa yanayohusiana na kutumia Maji yasiyo salama (*Waterborne diseases*) ikiwa ni pamoja na magonjwa ya Milipuko. Juhudi za kuondoa Majitaka katika miji yetu bado ni ndogo sana. Mamlaka zinatakiwa kuandaa mipango ya muda mfupi na muda mrefu katika kulishughulikia suala hili. Mamlaka zishirikiane na Halmashauri za miji husika hata ikiwezekana kununua magari ya kubeba majitaka yatakayotumika kuondoa Majitaka katika maeneo ambayo hayajafikiwa na mtandao wa bomba la majitaka ili kuweza kupunguza kutapakaa kwa majitaka katika maeneo tunayoishi. Vilevile, Mamlaka zihakikishe zinamiliki maeneo ya kutosha kwa ajili ya kujenga mabwawa ya kutibu majitaka mpango ambao unatakiwa uende sambamba na kasi ya kupanuka kwa miji yetu.

Ndugu Wajumbe, Katika Mkutano huu, msukumo (*thrust)* ya majadiliano pamoja na tathmini ya mwaka 2007/2008 ni Maji na Mazingira. Naamini tutajadili kwa kina zaidi kuhusu hali halisi

ya vyanzo vyetu vya maji katika kila mamlaka, mazingira yaliyopo, udhibiti wa majitaka katika maeneo yanayosimamiwa na mamlaka, usimamizi wa miradi inayoendelea kama inafanyiwa tathmini ya mazingira (EIA), changamoto zilizopo na hatua zitakazochukuliwa kukabiliana na changamoto zilizopo. Baada ya mkutano huu, naamini kila moja wetu atakuwa ameelewa zaidi majukumu yake katika kulinda na kutunza mazingira.

11. Shukrani kwa Wafadhili Waliochangia Mafanikio kwa Mwaka 2007/2008

Ndugu Wajumbe, Mafanikio haya tunayojivunia sasa yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na michango kutoka kwa nchi marafiki na taasisi zake. Ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa wote waliohusika kwa njia moja ama nyingine kuleta mafanikio haya. Miongoni mwao ni serikali ya Ujerumani kupita Mashirika ya Maendeleo ya GTZ na KfW, Shirika la Maendeleo la Denmark, Shirika la Maendeleo la Ufaransa, Shirika la Maendeleo la Norway, Shirika la Maendeleo la Uswisi, Shirika la Maendeleo la Japan, Shirika la Ufundi la Ubelgiji, Shirika la Milenia la Marekani, Shirika la Makazi Duniani, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika Benki ya uwekiezaji ya Nchi za Ulaya, pamoja na wengine wengi ambao wamekuwa wakichangia katika kuhakikisha sekta ya Maji inakuwa endelevu.
Nawashukuru sana na naomba muendelee na moyo huo.

11. Hitimisho

Mwisho nawashukuru wote waliohusika katika maandalizi mazuri ya Mkutano na pia kwa usikivu wenu. Ni matumaini yangu kwamba mengi yatajadiliwa katika mkutano huu ikiwa ni pamoja na mikakati madhubuti ya kupambana na changamoto zinazoikabili Sekta yetu ya Maji ambayo ni muhimu katika maendeleo na ustawi wa Taifa letu.

Naomba kwa umoja wetu tushirikiane kuendeleza Mamlaka za maji nchini ili ziweze kufikia Malengo ya Taifa katika Sekta ya Maji na azma ya Mamlaka zetu kujiendesha kwa kujitegemea (*Full Cost Recovery*). Nazitakia kila la kheri Bodi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Mamlaka za Maji nchini katika kuhakikisha tunawapatia wananchi huduma zilizo bora, zenye uhakika na endelevu kwa gharama nafuu.

Maji ni Uhai na Usafi wa Mazingira ni Utu

Asanteni kwa kunisikiliza